Wafanyakazi wazidi kulia makali ya kodi ya mshahara

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAKATI serikali ikiendelea na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2019/20, Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), kimetoa mapendekezo mbalimbali ikiwamo kufanyika mapitio ya makato ya kodi ya mshahara (PAYE) ili kutoa nafuu kwa mfanyakazi.

Mapendekezo hayo yalitolewa jana na Mwenyekiti wa THTU, Dk. Paul Loisulie, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya chama hicho kupitia kamati ya uchambuzi na ushauri kuandaa mapendekezo kuhusu bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema katika bajeti ijayo, wanashauri yafanyike mapitio katika viwango vya kodi vya mtu binafsi inayohusiana na PAYE ili kumpatia mfanyakazi unafuu wa kodi.

"Mapendekezo yamezingatia mfumo wa kodi wa nchi zingine za Afrika Mashariki na kusini mwa jangwa la Sahara na pendekezo mahususi linalotolewa ni kupandisha kima cha chini kisichokatwa kodi kutoka Sh. 170,000 hadi Sh. 360,000, hatua ambayo itapunguza maumivu ya kodi kwa mfanyakazi," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, katika kima cha chini cha mapato yasiyozidi Sh. 170,000 hakuna kodi inayokatwa, lakini mapato yanayozidi kiwango hicho hadi Sh. 360,000 kodi inayokatwa ni asilimia tisa.

Pia alisema mapato yanayozidi

INAENDELEA UK. 8